# HALMASHAURI YA MJI KONDOA

HABARI ZA WIKI

TOLEO NA:2

JUMATATU, JAN 30-FEB 05, 2023


## ARDHI



### RAIS AMALIZA MGOGORO WANANCHI NA GEREZA LA KING'ANG'A

Na. Sekela Mwasubila, Kondoa Mji

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amemaliza mgogoro wa ardhi wa muda mrefu kati ya wananchi wa Kata ya Kingale na gereza la King'ang'a uliodumu kwa zaidi ya miaka 30 kwa kugawa eneo lililokuwa linagombaniwa nusu kwa nusu.

Tamko la kumaliza mgogoro huo lilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhe. Ahmad Masauni wakati wa mkutano na wananchi wa Kata ya Kingale uliofanyika katika kata hiyo hivi karibuni.

"Leo hii tumekuja na habari njema kwa wana Kingale kuwa Rais ametoa suluhu kwa wananchi wa Kingale, ukiacha historia ya ukubwa wa eneo lililokuwa lina mgogoro kati ya magereza na wananchi wa Kingale ambalo lilikuwa na ukubwa wa ekari 7,495.74. Mhe. Rais ameelekeza ekari 3,272.4 zibaki kwa wananchi na kuendelea kulitumia kwa shughuli za kilimo na mifugo na shughuli zingine za kiuchumi," alisema Mhe. Senyamule.

YALIYOMO NDANI


**WAKULIMA WALIOKOSA NAMBA MBOLEA YA RUZUKU WATAKIWA KUTOKAA KIMYA UK. 4**

**RC SENYAMULE ATAKA WATENDAJI KUFUATILIA WANAFUNZI AMBAO HAWAJARIPOTI SHULE UK. 5**

**WANAFUNZI KIDATO CHA KWANZA WAFUNDWA UK. 6**

**WANANCHI WATAKIWA KUTOWEKA TAKATAKA BARABARANI UK.7**



INATOKA UK 1

## RAIS AMALIZA MGOGORO WANANCHI NA GEREZA LA KING'ANG'A

Aidha, liongeza kuwa ekari zinazibaki zibaki kwa ajili ya matumizi ya Magereza kwa shughuli zao zote ambalo ni karibu ya nusu ya eneo. Alisema kuwa uamuzi huo umedhihirisha kuwa Mhe. Rais yupo kwa ajili ya wananchi kwa kuwa angeweza kusema kwasababu eneo hilo limekuwa linatumiwa na Magereza kwa kipindi kirefu basi lingebaki kwa Magereza.

"Eneo hili baada ya kutolewa inatakiwa kufanyika mambo yafuatayo, kwanza watu wa ardhi ndani ya mwezi mmoja waje wafanye utaratibu wa kuonesha mipaka halisi ya maeneo yalivyogawanywa kwa kushirikiana na Magereza wenyewe pamoja na viongozi wa vijiji. Eneo lipimwe na liwekwe mipaka halisi na ziwekwe bikoni kubwa na zionekane na kila mmoja," alisisitiza Mhe. Senyamule.

Aliwataka viongozi wa maeneo hayo kuendelea kutunza mipaka ili kuzuia muingiliano ikiwa ni pamoja na Magereza kuwashauri Wizara ya Kilimo kuweka utaratibu wa kuweka bwawa kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji kwa kuwa eneo hilo ni bonde na Wizara ya Mifugo kujenga majosho na mabwawa kwa ajili ya kunyweshea mifugo ya wananchi wa kata ya Kingale.

Akiongea wakati wa mkutano huo, Mbunge wa Jimbo la Kondoa Mjini, Mhe. Ally Makoa alisema mapendekezo yaliyotoka kwa wananchi ya kilometa 1.5waachiwe Magereza na kilometa 1.5 Kambi ya Moto hadi kwenye Mbuyu. Hivyo, wao wataendelea na eneo lao la kilometa ambalo hajawalima ambalo kwa sasa ni wazi na walipokuwa wakiingiza mifugo yao walikuwa wanakamatwa.

"Shukrani kubwa kwa Mhe. Rais na wizara ni kutuleta wataalam kutoka Wizara ya kilimo kwa ajili ya kutuwekea miundombinu ya umwagiliaji katika eneo lile ili tunyweshwe mifugo yetu na tulime tumwagilie wakati wote na mkumbuke hii ni Halmashauri ya Mji kuna wakati Mkurugenzi atazuia kulima na ndio maana tunaweka kulimo cha mjini," alisisitiza Mhe. Makoa.

Mwakilishi wa wananchi wa Kingale alimshukuru Mhe. Rais kwa kuwapatia eneo lililokuwa linangojewa kwa muda mrefu na kumuomba mkuu wa mkoa kuwataka wataalam wa ardhi kwenda haraka kwa kuwa wapo na wazingatie maagizo ya Mhe. Rais kuhusu mipaka.

Mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa Kata ya Kingale na Gereza la King'ang'a ulidumu kwa zaidi ya miaka 30 ambapo eneo lililokuwa linagombaniwa lilikuwa na ukubwa wa ekari 7495.74.



## KILIMO, MIFUGO NA UVUVI




# WAKULIMA WALIOKOSA NAMBA MBOLEA YA RUZUKU WATAKIWA KUTOKAA KIMYA

Na. Sekela Mwasubila, Kondoa Mji

Wakulima waliojiandikisha kwenye daftari la kupata mbolea ya ruzuku ya serikali wametakiwa kutokaa kimya wanapopata changamoto ya kupata mbolea hiyo badala yake wawatumie maafisa ugani wa maeneo yao ili kuhakikisha wanapata mbolea.

Wito huo ulitolewa na Kaimu Afisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Mji Kondoa, Ndg. Severin Lyimo alipokuwa akifanya mahojiano na wanahabari ofisini kwake hivi karibuni.

“Kuna wakati baadhi ya wakulima hawakupata namba kutokana na mfumo kucheza, lakini hiyo haiwanyimi fursa ya wao kupata mbolea sababu waliojiandikisha sisi tunawaangalia kwenye mfumo tunawapatia namba wanapata mbolea,” alisema Lyimo.

Alisema kuwa ili mkulima apate mbolea anapaswa awe alikwishajiandikisha kwenye daftari ambapo huingizwa taarifa kwenye mfumo na anatumiwa namba maalum kwenye simu yake.

Namba hiyo anapaswa kufika nayo kwenye kituo cha kuuzia mbolea na kuingizwa kwenye mfumo na atapewa mifuko ya mbolea kulingana na ukubwa wa shamba lake alilojiandikisha awali.

“Kuna changamoto kidogo ilijitokeza sijui ni kukosa uelewa kwa baadhi ya wakulima hawakuwa na simu walitumia namba za simu za watu wengine kama jirani zao. Lakini mwisho wa siku wanakuja wanasema hawakupata namba sisi tunachofanya ni kuwaangalia kwenye mfumo kama kweli ni yeye kama ni yeye tunaweka namba ya simu ambayo atakuja nayo,” alisisitiza Lyimo.

Pia aliongeza kwa kuwataka wakulima kununua mbolea ya ruzuku kwa wakati ili kuepuka changamoto ya wengi wao kuulizia mbolea inapoisha.
Alisema kuwa mbolea inapofika wengi hawafiki katika kituo cha kuuzia mbolea na kuishia kulalamika mitaani kuwa mbolea haipo na taarifa ya uwepo wa mbolea hutolewa na maafisa ugani katika maeneo yote.

Halmashauri ya Mji Kondoa hadi sasa imepokea mbolea ya ruzuku ya kupandia na kukuzia tani 150, mbolea ya kukuzia ipo inauzwa katika maghala yaliyopo Mtaa wa Bicha kwa bei elekezi ya shilingi 70,000 na serikali imeshalipa fedha nyingine.



## ELIMU



## RC SENYAMULE ATAKA WATENDAJI KUFUATILIA WANAFUNZI AMBAO HAWAJARIPOTI SHULE

Na. Alex Sona, Dodoma

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule amewataka watendaji wa kata za Viwandani, Chadulu, Makole na Hazina kuhakikisha wanafatilia wanafunzi ambao hawajaripoti shule wakahakikiwe kama wamefika shuleni hata kama wapo shule binafsi ili mradi wawe shule.

Aliyesema hayo Februari 03,2023 jijini Dodoma katika shule ya sekondari Viwandani wakati akikagua maendeleo ya wanafunzi walioripoti shuleni pamoja na kuzungumza na watendaji wa kata hizo kutokana na shule hiyo kuwa na wanafunzi wa chache walioripoti.

Aidha aliwakata watendaji kuendelea kutekeleza sera ya kukijanisha Dodoma nakuhimiza kila kaya upanda miti na taasisi zote zinazozungukia kata yake na kuhimiza kupanda kwa kupendezesha yaani kwa mpangilio.

“Nendeni mkahakiki nakuleta ripoti ya wanafunzi ambao bado hawajafika shule kwa kata zote na kwa shule binafsi kuhakikisha taarifa zao kama wameenda shule cha muhimu mwanafunzi awe shule hata kama yupo shule binasfi haina tatizo,”alisema Mhe. Senyamule

Pia mnawajibu wa kuendelea kuwaambia wananchi kuhusiana na masuala ya kukijanisha Dodoma kwa kila kaya na taasisi zote wanatakiwa kupanda miti 5 na kuhakikisha wanapanda kwa mpangilio,”alisema Mhe. Senyamule.

Mhe.Senyamule alishiriki pia katika zoezi la upandaji miti katika shule hiyo yote ikiwa ni kuendeleza utekelezaji wa kukijanisha Dodoma.

Kwa upande wake Afisa Mtendaji wa Kata ya Viwandani Tumi Dachi alimwaomba Mkuu wa mkoa kuwasaidia kuwaondoa wafanyabiashara waliozunguka kwa kuwa wanawachanganya wanafunzi.



## ELIMU SEKONDARI



# WANAFUNZI KIDATO CHA KWANZA WAFUNDWA

Na. Sekela Mwasubila, Kondoa Mji

Wanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Ula Halmashauri ya Mji Kondoa wametakiwa kuwa na nidhamu na kuzingatia sheria za shule walizopewa ili kuwa wanafunzi bora na kufanya vizuri katika masomo yao.

Agizo hilo lilitolewa na Afisa Elimu Sekondari, Mwalimu Annette Nara alipokuwa akiongea na wanafunzi wa kidato cha kwanza waliopo katika shule hiyo wakati wa ziara ya ufuatiliaji aliyoifanya shuleni hapo.

“Kufaulu wote inawezekana ila ni jitihada zako mwenyewe, kikubwa unapaswa kutunza nidhamu yako na kuepuka kujiingiza kwenye makundi ya utoro, ulaji wa mirungi na uvutaji wa bangi hayatakusaidia zaidi utapotea na ndoto zako,” alisema Mwalimu Nara.

Aidha, aliwaambia kuwa wakifanya makosa ya utovu wa nidhamu watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria za shule ambazo wanatakiwa kuzishika vizuri ili wapate matokeo mazuri. Aliwakumbusha kuwa hawakufaulu kwa bahati mbaya bali walifaulu ili waweze kutimiza ndoto zao.

“Afisa elimu huyo aliwataarifu kuwa Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amepeleka fedha kwa ajili ya mradi wa maji, kujenga madarasa mazuri na walimu wa kutosha. Aliwataka kuhakikisha wanasoma kwa bidii na kupata daraja la kwanza na la pili.

“Na nyie watoto wa kike ni marufuku kuvua sketi zenu kwa vijana huko mitaani na tukikujua umevua utalala gerezani kwa kuwa unakuwa umetutia aibu. Wasichana wote mlindane wenyewe mkiona mwenzenu anakuwa na tabia mbaya toeni taarifa kwa mkuu wa shule na nyie wavulana mtusaidie kuwalinda dada zenu kwa kuwa hapa kazi ni moja tu ya kusoma,” alisisitiza Mwalimu Nara.

Shule ya Sekondari Ula ipo katika Kata ya Kondoa Mjini kwa mwaka 2023 imepangiwa wanafunzi 309 na hadi kufikia tarehe 1 Februari, 2023 wanafunzi 234 walikuwa wameripoti, wanafunzi 25 walihama na jitihada za kuwatafuta waliobakia zinaendelea.



## ZIARA YA SEKRETARIETI YA MKOA



# “KALAMU NI JEMBE LISILOUMIZA MIKONO”- AFISA ELIMU MKOA

Na. Sekela Mwasubila, Kondoa Mji

Afisa Elimu Mkoa wa Dodoma, Mwalimu Gift Kyando amewaambia wanafunzi kuwa kalamu ni jembe la mtaani lisiloumiza hivyo wasome kwa bidii walitumie ili wasije kukutana na jembe linaloumiza mikono.

Kauli hiyo aliitoa wakati akizungumza na wanafunzi wa darasa la Nne katika Shule ya Msingi Kolowasi alipotembelea shuleni hapo wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa shuleni hapo.

Mwalimu Kyando alisema “someni kwa bidii ili baadae muwe na maisha mazuri, hamtamani kuwa kama afisa elimu yule pale, basi someni kwa bidii wanangu wazuri hii ni kalamu ila huko mtaani ni jembe lisiloumiza mikono saa hizi baba na mama wanatumia hili jembe, hawatumii hili wanatumia ambalo mbavu na mikono vinauma”.

Aliwaeleza kuwa wanapaswa kuwasikiliza walimu, kutotoroka shuleni na kuuliza pale ambapo hawaelewi hata kwa rafiki zao. Aliwataarifu kuwa kufanya hivyo, wote watafaulu mtihani wao na kuingia shule za Sekondari na vyuo na wakimaliza watakuwa na taaluma zao zinazoeleweka.

“Na mjue wanangu wazuri mtu anayepata taabu duniani ndiye atakayepata taabu na mbinguni. Hivi nilivyo naweza kutamani kitu cha mtu? Anayetamani kitu cha mtu ni maskini. Hivyo, someni nenda mkamwambie baba na mama wawaache msome. Nawatakia kila la kheri katika masomo yenu,” alisema Mwalimu Kyando.

Viongozi wa mkoa wamefanya ziara ya ukaguzi wa miradi ndani ya Halmashauri ya Kondoa Mji kwa siku mbili ambapo walitembelea miradi ya afya, elimu na maendeleo ya jamii ili kujionea namna miradi hiyo inavyotekelezwa na hatua iliyopo.



## USAFI WA MAZINGIRA



# WANANCHI WATAKIWA KUTOWEKA TAKATAKA BARABARANI

Na. Sekela Mwasubila, Kondoa Mji

Wananchi wa Halmashauri ya Mji Kondoa wametakiwa kuacha tabia ya kutoa takataka barabarani kabla gari la matangazo halijapita kuwatangazia kuwa ni zamu yao gari la kukusanya taka kupita hali ambayo itauweka mji kuwa katika hali ya usafi.

Kauli hiyo ilitolewa na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mazingira na udhibiti wa taka ngumu Halmashauri ya Mji Kondoa, Ndg. Alfred Chakalike alipokuwa akielezea mipnago ya kuuweka safi Mji wa Kondoa ofisini kwake.

“Nawasihi sana wananchi wazingatie ratiba ya gari la uzoaji taka katika mitaa yao ikiwa ni pamoja na kuchangia ada za usafi kila mwezi pamoja na taasisi ili taka zizolewe kwa wakati. Hadi sasa wanaochangia ni wachache na kupelekea uendeshaji kuwa mgumu kwa watendaji,” alisema Chakalike.

Aidha, aliwataka watendaji wa mitaa na kata pamoja na kamati za mazingira kusimamia kwa kufanya doria katika mitaa yao dhidi ya vitendo vya utupaji taka katika maeneo ya wazi, vichochoroni na katika maeneo ya vyanzo vya maji.

Aliongeza kwa kuwataka kuwakumbusha wananchi kufanya usafi katika maeneo yao kila siku na si kusubiria hadi Jumamosi ya mwisho wa mwezi na wafanye usafi kwa kufeka nyasi ikiwa ni pamoja kufanya usafi katika maeneo yasiyoendelezwa na mapagale.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kuzingatia kuwa kufanya usafi ni jukumu la kila mmoja katika eneo lake na kwa wote ambao watakaidi kufanya usafi wa mazingira Halmashauri ya Mji Kondoa itachukua hatua za kisheria dhidi yao kwa kutozwa faini ya shilingi 50,000.





# TAARIFA MBALIMBALI/MATANGAZO YA IDARA

## UHUISHAJI WA LESENI ZA BIASHARA

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA ANAWAKUMBUSHA WAFANYABIASHARA WOTE WA KONDOA MJI KUHUISHA LESENI ZA BIASHARA KWA ZILIZOKWISHA MUDA NA ZINAZOKARIBIA KUMALIZA MUDA WA MATUMIZI.

AIDHA WOTE AMBAO WATAKUTWA BILA LESENI AU ZIMEKWISHA MUDA WATALIPA ASILIMIA 20 YA BEI YA LESENI YA BIASHARA WANAYOFANYA.

USOMAPO TANGAZO HILI MJULISHE NA MWENZAKO

## UCHUKUAJI WA FOMU ZA VIBANDA STENDI YA MABASI BICHA

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA ANAWAKUMBUSHA WANANCHI WOTE NA WAFANYABIASHARA WALIOOMBA KUJENGA VIBANDA VYA BIASHARA KATIKA STENDI KUU YA MABASI BICHA KUFIKA KATIKA OFISI ZA BIASHARA KARIBU NA JENGO LA CRDB KWA AJILI YA KULIPIANA KUCHUKUA FOMU ZA MAOMBI KWA AJILI YA KUENDELEA NA TARATIBU ZINGINE

AIDHA IKUMBUKWE KUWA AMBAO HAWATAFIKA KULIPIA FOMU HIZO NAFASI HIZO WATAPEWA WAOMBAJI WENGINE.

USOMAPO TANGAZO HILI MJULISHE NA MWENZAKO

## ULIPIAJI WA TOZO ZA TAKA

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WA KONDOA MJI KULIPA TOZO KWA AJILI YA HUDUMA YA UBEBAJI WA TAKA KATIKA MITAA YAO.

AIDHA ANAWATAKA KUFANYA USAFI KWA KUZIBUA MITARO ILI MAJI YA MVUA YAKIJA YAPATE SEHEMU ZA KUPITA IKIWA NI PAMOJA NA KUPIGA MARUFUKU WANANCHI KUTUPA TAKA KATIKA MITARO.

PIA WANANCHI MNATAKIWA KUFANYA USAFI KATIKA MAENEO YANAYOWAZUNGUKA NA MAPAGARE KWA KUFYEKA NYASI.

WATAKAOKUTWA WANATUPA TAKA MITARONI NA AMBAO HAWAJAZIBUA MITARO FAINI NI SHILINGI ELFU HAMSINI.

USOMAPO TANGAZO HILI MJULISHE NA MWENZAKO

# MIRADI MBALIMBALI ILIYOTEMBELEWA NA SEKRETARIETI YA MKOA




MAABARA SHULE YA SEKONDARI KOLO




KITUO CHA AFYA KOLO




KIKUNDI CHA WANAWAKE BICHA




UJENZI WA WODI HOSPITALI YA MJI